

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

614

MAARIFA YA JAMII

Muda: Saa 3

Alhamisi, 07 Mei 2015 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** katika kila sehemu B na C.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Andika majibu yako kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
5. Vikokotozi na Simu za mkononi **haviruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

1. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya "vitangulizi vya ukoloni."
(b) Bainisha vitangulizi vitatu vya ukoloni katika Afrika.
2. Bainisha sababu nne zilizofanya kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni katika Afrika.
3. Eleza kwa kifupi aina na athari za mizunguko ya dunia.
4. Badilisha vipimo vya ramani vifuatavyo kuwa katika sentensi ukitumia Kilometa.
(a) 1: 25 000 000 (b) 1: 200 000
5. Bainisha changamoto nne zinazokabili umoja wa Afrika hadi sasa.
6. Toa tathmini fupi ukionesha mambo manne yanayobainisha umuhimu wa mkutano wa Berlin kwa mataifa ya Ulaya uliofanyika katika karne ya 19.
7. Eleza kwa ufupi sifa nne zinazobainisha mfumo wa uzalishaji wa ujima.
8. Eleza kwa kifupi vipengele vinne vya tabia nchi.
9. Orodhesha na kuelezea kazi za vipengele vyovyote vinne muhimu vya ramani.
10. Bainisha athari nne za ufugaji holela katika mazingira ya Tanzania.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu swali moja (1) kutoka katika kila kipengele.

Kipengele I: Jiografia

11. "Shughuli za kibinadamu ndiyo pekee huathiri tabia nchi ya eneo." Jadili.
12. Tathmini madhara matano yanayotokana na uchimbaji wa madini katika Afrika Mashariki.

Kipengele II: Historia

13. Eleza tofauti tano kati ya Mfumo wa Zama za Mawe na mfumo wa Zama za Chuma.
14. Fafanua mbinu tano zilizotumika kuimarisha utawala wa kikoloni katika Tanganyika.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu swali moja (1) kutoka katika kila kipengele.

Kipengele I: Jiografia

15. Fafanua hatua ambazo mwalimu anatakiwa kufuata endapo atatumia Redio kama zana ya kufundishia somo la Jiografia.
16. Tathmini faida za matumizi ya njia shirikishi katika kufundisha somo la Jiografia.

Kipengele II: Historia

17. Eleza kwa kina faida tano za matumizi ya ziara kama mbinu ya kufundishia somo la Historia.
18. Eleza kazi za upimaji na tathmini katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Historia